Kuridhika

na

Terry Warford

Kuridhika

na

Terry Warford

Novemba 5, 2011

Kuridhika

Kwanzia mwanzo wa nyakati, mwanadamu hajawahi kuridhika na kile anachokitoa Mungu. Mungu alifanya ulimwengu mzuri, na uliokamilika na akaiona kuwa ni nzuri. Alifanya bustani katika ulimwengu huo, na akamweka mwanamume na mwanamke katika bustani hiyo ili aitunze na afurahiye.

Pamoja na baraka zote ambazo Mungu alizitoa, Adamu na Hawa hawakuridhika. Mwanzo 3:1-6 inatuambia hadithi ya kusikitisha, "*Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, matunda ya miti ya bustani twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe naye akala.*" Shetani aliwajaribu ili wasiridhike. Alichowapa Mungu hakikuwa kinawatosha. Walitaka kuwa kama "miungu" na wakaleta dhambi na kifo katika ulimwengu ambayo Mungu aliwapa. Walitaka mengi lakini wakaishia kwa machache.

Kuwa na shukurani na kuridhika (furaha) na kile ambacho Mungu ametoa ndiyo ufunguo mkuu wa kuishi maisha ya Kikristo. Tusiporidhika, tuko katika, hatari, ya kusema kwamba alichutupatia Mungu siyo nzuri sana. Hebu tusimtukane Mungu kiivyo. Hebu na turidhike na tuwe na shukurani, tukimshukuru Mungu kwa zawadi yake kuu.

Hebu tuangalie katika baadhi ya sehemu ya maisha yetu ya Ukristo ambayo kuridhika kunaendana nayo.

Kuridhika na vitu ambavyo Mungu ametupatia

Katika Luka 3:10-14 tunasoma mafundisho ya Yohana mbatizaji katika kuridhika, "*Makutano wakamwuliza tufanye nini basi? Akawajibu akiwaambia, mwenye kanzu mbili na ampe asiye na kanzu; na mwenye chakula na afanye vivyo hivyo. Watoza ushuru nao wakaja kubatizwa, wakamwuliza mwalimu tufanye nini sisi? Akawaambia msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa. Askari nao wakamwuliza, wakisema, sisi nasi*

tufanye nini? Akawaambia msidhulumu mtu, wala msishitaki uongo; tena mtosheke na mshahara wenu."

Kila kikundi kiliamuriwa kiridhike. Watu waliokuwa na kanzu mbili au chakula kingi wasingepaswa kufikiria kupata zaidi, bali wagawane. Watoza ushuru hawakupaswa kuwaibia watu tofauti na kile walichoamuriwa. Na askari nao walipaswa kuridhika na mishahara yao. Yote haya pia yanatulenga hata sisi pia.

Tusiwe na tamaa, turidhike. Ebr. 13: 5, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.*"

Tuwe waaminifu, turidhike. 1 Pet. 2:12, "*Mwe na mwenendo mzuri kati ya mataifa, ili iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.*"

Turidhike na mishahara yetu. 1 Tim. 6:6-8, "*Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatu kuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na nguo na chakula tutaridhika na vitu hivyo.*" Mistari ya 9-10 alafu inatuonya kuhusu hatari ya kutokuridhika, "*Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. Maana shina moja la mabaya ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivi mengi.*"

Katika Fil. 4:13, mtume Paulo aliandika, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*" Wanadamu wakati mwingine hutumia kifungu hiki kwa kusema tunaweza kupata mali yo yote tunayotaka, lakini kimsingi Paulo anaitumia katika mazingiza ya kuwa radhi. Mistari ya 11-13, "*Si kwamba nasema haya kwa kuwa nina mahitaji; maana nimejifunza kuwa radhi na hali yo yote niliyo nayo. Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na wingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.*"

Katika Mt. 6:31-33 Yesu anatukumbusha kwamba tusihofu kuhusu vitu. Tunapaswa kuridhika kwa sababu Mungu atatujali. "*Msisumbuke basi mkisema tule nini? Au tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yoye mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Sawa, pesa zetu na vitu siyo sehemu pekee ya maisha yetu ambayo tunahitaji kuridhika navyo. Hebu tuangalie sehemu nyingine.

Turidhike na wenza wetu

Mhu. 9:9, "*Uishi kwa furaha pamoja na mke umpendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, ulizopewa chini ya jua; siku zote za ubatili wako, kwa maana huo ni sehemu yako ya maisha; na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya jua.*" Sehemu yetu ni wenza wetu wenyewe, na kuishi kwa furaha na mtu huyo. Siyo mwingine, au kushawishiwa na wengine. Tena, kama hatuna furaha na wenza wetu, tunasema kwamba zawadi ya Mungu siyo nzuri vya kutosha. Mith. 18:22, "*Apatae mke apata kitu chema; naye ajipatia kibali kwa BWANA.*"

Katika Mith. 5:15 tunasoma kwamba, "*Unywe maji ya birika lako mwenyewe na maji yenye kububujika katika kisima chako.*" Katika mustari huu anaongelea mwanamke na mwanamume. Kumbuka mustari wa 18, "*Chemchemi yako ibarikiwe; nawe umfurahie mke wa ujana wako.*" Mustari wa 20 unauliza, "*Mwanangu mbona unashangilia Malaya, na kukikumbatia kifua cha mgeni?*" Tukiligeukia lingine inatuongoza katika kifo, mustari wa 23, "*Atakufa huyo kwa kukosa maonyo, naye atapotea kwa wingi wa ujinga wake.*"

Katika Mt. 5:27-28, Yesu anatumia uzinzi sio tu katika miili yetu, bali pia katika macho yetu na mioyo yetu pia. "*Mmesikia kwamba imenenwa, Usizini; lakini mimi nawaambia kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.*"

Hebu na turidhike na wenza wetu, na kumshukuru Mungu kwa zawadi yake.

Turidhike na Kanisa Lake Kristo

Katika Mt. 16:15-18, Yesu anawauliza wanafunzi wake, "*Akawaambia nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani? Simoni Petro akajibu akasema , wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai. Yesu akajibu akamwambia, heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni. Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Kwa vile Yesu Kristo alilijenga kanisa lake mwenyewe, kwa nini tunajaribu kufuata makanisa mengine ya wanadamu, au tunaanzisha letu wenyewe? Na ni wangapi wanaofanya sawasawa?

Yesu alilifia kanisa lake, ili aweze kujiletea kanisa linalo pendeza lake binafsi. Efe. 5: 25-27, "*Enyi waume wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo*

na hila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa."

Kanisa lake Kristo ni mwili wake. Kol. 1:18, inamuongelea Yesu, soma, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*" Efe. 1: 22-23, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Ni mwili wake, ambalo ndiyo kanisa lake, ambalo tunabatizwa kwalo, 1 Kor. 12:13, "*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.*" Hivyo, katika kanisa lake sisi ni viungo vya mwili wake. Mustari wa 12 unasomeka hivi, "*Maana kama vile mwili ni mmoja nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo.*" Mustari wa 27, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo na viungo kila kimoja peke yake.*"

Kanisa lake Kristo lilianzishwa na wanafunzi wake (na hivyo likajengwa na Yesu Kristo) siku ya Pentekoste, soma sura ya kwanza na pili ya kitabu cha Matendo ya Mitume. Wanafunzi wake walikuwa wa kanisa la Kristo na wakatambuliwa hivyo, Rum. 16:16, "*Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*" Hivyo tunapokuwa washirika wa mwili wake , tunakuta kwenye Efe. 2:19-20, "*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa Mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.*"

Kwa nini tugeukie katika kanisa tofauti? Je inaweza ikawa kwamba tunatamani kuwa kama Adamu na Hawa "*kama miungu*"? ni ukatili wa aina gani. Hebu na tunyenyekee, na turidhike na kanisa ambalo Yesu alijenga. 1 Pet. 5:6, "*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake.*"

Turidhike na Neno La Mungu

Mitume walipokuwa wakianzisha kanisa la Kristo pia walikuwa wanatoa neno la Mungu kwa wanadamu. Yesu kwanza aliwapatia neno la Mungu wakati wa huduma yake na baada ya kufufuka kwake kutoka katika wafu. Mdo. 1:1-3, "*Kitabu kile cha kwanza nalikiandika Theofilo, katika habari ya mambo yote aliyoanza Yesu kufanya na kufundisha, hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha kuwaagiza Roho Mtakatifu wale Mitume aliowachagua; wale aliowadhirishia nafsi yake,*

kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu."

Roho Mtakatifu akawakumbusha Mitume kile alichokifundisha Yesu, na kuwaongoza katika kweli yote. Katika Yoh. 14:26, "*Lakini huyo msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwa kumbusha yote niliyowaambia.*" Yoh. 16:13, "*Lakini Yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*"

Yesu hajawahi kuniambia kitu ana kwa ana. Roho Mtakatifu asingekuwa na kitu cha kunikumbusha. Roho aliwaongoza mitume katika kweli yote. Je hiyo imeniachia nini?

Alafu mitume wakafundisha neno la Mungu, na wakaiandika kwa ajili yetu, ili tuweze kuwa nayo hata baada ya kufariki kwao. Katika 2 Pet. 1:12-15, mtume Petro aliandika, "*Kwa hiyo nitakuwa tayari kuwa kumbusha hayo siku zote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo. Nami naona ni haki maadamu nipo mimi katika maskani hii, kuwaamsha kwa kuwakumbusha. Nikijua kwamba kule kuwekea mbali maskani yangu kwaja upesi, kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyonionyesha. Walakini nitajitahidi, kwamba kila wakati baada ya kufariki kwangu mpate kuyakumbuka mambo hayo.*" Na akaendelea katika 2 Pet. 3:1-2, "*Wapenzi waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi; katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa kuwa kumbusha, mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na ile amri ya Bwana na Mwokozi iliyoletwa na mitume wetu.*". Mtume Paulo akaandika katika 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona ya kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*" 2 Pet. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*"

Sasa kwa nini tugeukie njia zetu wenyewe? Kwa nini tusiridhike, na neno la Mungu kama lilivyotolewa? Kuwa kama "*miungu*" sisi wenyewe? Hebu na tusiwe wapumbavu. Mith. 28:26, "*Mwenye kujitumainia moyo wake ni mjinga; bali yeye aendaye kwa busara ataokolewa.*"

Tunatembeaje kwa busara? Kwa kusikia na kufanya neno la Mungu. Katika Mat. 7:24 Yesu alisema, "*BAsi kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba.*"

Katika Yoh. 8:31-32 tunakuta kwamba, "*Basi Yesu akawaambi wal Wayahudi waliomwamini, ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa*

*wanafunzi wangu kweli kweli;"*hebu na turidhike na neno la Mungu, na kushukuru kwalo.

Tunajengaje kuridhika katika maisha yetu?

Hapa kuna njia za haraka:

Shukurani

Tambua zawadi za Mungu kama hiyo, na kuonyesha shukurani kwa hayo. Zab. 100:3-5, "*Jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake; kwa kuwa BWANA ndiye mwema; Rehema zake ni za milele; na uaminifu wake vizazi na vizazi.*"

Upole

Usijaribu kuwa kama "*miungu*". Jaribu kumtumikia Mungu mmoja na aliye hai. Yakobo 4:6-8, "*Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu. Basi mtiini Mungu. Mpingeni shetani, naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili.*"

Tumtumikie Mungu kwa juhudi zetu bora

Tusifanye mambo kwa njia zetu wenyewe. Badala yake tumpe Mungu juhudi zetu bora. Zab. 119:2-3, "*Heri wazitiio shuhuda zake, wamatafutao kwa moyo wote. Naam, hawakutenda ubatili, wamekwenda katika njia zake.*" Unaona tukimtafuta kwa mioyo yetu yote tunatembea katika njia zake, siyo njia zetu? Huko ni kuridhika. Fil. 4:4, "*Furahini katika Bwana siku zote, tena nasema furahini.*"

Tutafute kukua katika Yeye

Lazima turidhike na vyote ambavyo Mungu ametupa. Kitu pekee ambacho hatutakiwi kuridhika nacho ni sisi ni wakina nani. Unatafuta kukua. Kumbuka tunavyosoma katika Fil. 4:12, kwamba Paulo alikuwa katika hali zote shibe na njaa, akiwa na mateso ya kifungo? Kama tukiridhika, tunahitaji nini au kukionea njaa? Kukua. 1 Pet. 2:2, "*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yalighoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu;*". 2 Pet. 3:18, "*Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*"

Kuna wimbo wa zamani usemao: Kuridhika kunatawala umilele mbinguni mji wetu mtamu mji.” Lazima ianzie hapa katika maisha haya.

Imetolewa kwa jina la Kristo,

Ndg. Terry Warford